**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**

**DIVISHENI YA KAZI**

**DAR ES SALAAM**

**MAOMBI YA ANUAI NA. 364 YA MWAKA 2019**

**KATI YA**

1. **DDI ATHUMAN SENYAGWA ........................................... MLETA MAOMBI**
2. **IDDY E. LAVILE ........................................................... MLETA MAOMBI**
3. **GODWIN J. SERASERA ................................................ MLETA MAOMBI**
4. **HARUNA IBRAHIM ...................................................... MLETA MOAMBI**
5. **CHARLES KADEGA ....................................................... MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**ESTIM CONSTRUCTION COMPANY...................................... MJIBU MAOMBI**

**UAMUZI**

Tarehe ya Amri ya Mwisho: 22/02/2021

Tarehe ya Uamuzi: 20/04/2021

**A. E. MWIPOPO, J.**

Waleta maombi Iddi Athumani Senyagwa, Iddy Lavile, Godwin Serasera, Haruna Ibrahim na Charles Kadega wameleta maombi haya wakiomba wapewe kibali na Mahakama hii kufungua shauri la pamoja (Representative suit). Maombi haya yameletwa chini ya kifungu cha 44(1) na (2) cha Kanuni za Mahakama ya Kazi, 2007.

Akitoa maelezo kwa niaba ya waleta maombi, Bw. Charles Kadega ameeleza kuwa waleta maombi walifungua shauri la pamoja mbele ya Tume ya Usuluhishi na Uamuzi lenye namba CMA/DSM/ILA/R.1017/16 ambapo hawakuridhishwa na uamuzi wa Tume. Hivyo, wanaomba wafungue shauri la marejeo la pamoja ambapo Iddi Athumani Senyagwa na Charles Kadega wameteuliwa na waleta maombi wenzao ili waweze kufungua shauri hilo kwa niaba yao. Wameeleza kuwa waleta maombi wenzao wametoa kibali ili waleta maombi tajwa hapo juu wawawakilishe na kufungua shauri kwa niaba yao.

Mjibu maombi katika shauri hili amesema kuwa hana pingamizi na maombi hayo.

Kanuni ya 44(2) ya Kanuni za Mahakama ya Kazi, Tangazo la Serikali Na. 106 la 2007, inataka pale kunapokuwa na mtu zaidi ya mmoja ambaye ana maslahi (interest) na shauri basi wanaweza kuchagua mmoja au baadhi yao kuwawakilisha baada ya kupata kibali cha Mahakama. Katika maelezo yao, Bw. Charles Kadega ameeleza kuwa walifungua shauri la pamoja mbele ya Tume na hawajaridhika na uamuzi ule, hivyo wanaomba Bw. Iddi Athumani Senyagwa na Bw. Charles Kadega wafungue shauri kwa niaba ya Waleta Maombi ili kuwawakilisha. Nimeangalia taarifa ya maombi (Notice of

Application) na "Chamber Summons" nimeona kuwa zinaonyesha waleta maombi wanataka kufungua shauri la pamoja (Representative Suit). Ingawa katika hati hizo hawaonyeshi ni nani waliyemteua kufungua shauri la pamoja kwa niaba yao ni wazi kuwa maombi yao ni kwa ajili ya kuteua baadhi yao kuwawakilisha. Nyaraka hizo zimesainiwa na waleta maombi wote watano. Hata hivyo, kiapo cha pamoja cha waleta maombi hakijajielekeza katika kutoa maelezo ya kuunga mkono maombi ya waleta maombi. Kiapo hicho kimejielekeza katika kubatilishwa kwa uamuzi wa Tume badala ya kujielekeza katika kuomba kibali cha kufungua maombi ya pamoja. Kwa kuwa waleta maombi sio wanasheria na hawana uwakilishi na kwa nia ya kutenda haki pamoja na mapungufu ya kiapo cha pamoja cha Waleta maombi ni wazi kuwa nia yao ni kufungua maombi ya pamoja.

Ni maoni yangu kuwa taarifa yao ya maombi inaonesha wazi kuwa waleta maombi wana maslahi ya pamoja inayotokana na shauri walilolifungua pamoja mbele ya Tume ambapo wanataka kupinga uamuzi huo wa Tume. Na kwa kuwa maombi hayo wameyaleta kwa pamoja na kuna saini zao inaonesha kuwa wamekubaliana kuwa Bw. Idd Athumani Senyagwa na Charles Kadega wafungue shauri la marejeo la pamoja kwa niaba yao.

Hivyo, naona kuwa waleta maombi wametimiza matakwa ya Kanuni ya 44(2) cha kanuni za Mahakama ya Kazi, 2007.

Hivyo, maombi haya yanakubaliwa. Waleta maombi wanapewa kibali cha kufungua shauri la pamoja. Bw. Iddy Athumani Senyagwa na Charles Kadega wanateuliwa kufungua shauri la pamoja kwa niaba ya waleta maombi wengine dhidi ya uamuzi wa Tume ya Usuluhishi na Uamuzi katika mgogoro Na. CMA/DSM/ILA/R.1017/16. kila upande utagharamia gharama zake za kuendesha shauri hili.

A.E. Mwipopo
**JAJI**
20/04/2021